

## Tessera yo Lejio Maria

### SALA ZA MWANZO

Kwa jina la Baba .....

Uje Roho Mtakatifu, uzienee roho za waumini wako, uwatie mapendo yako.

V. Peleka Roho yako, vitaumbwa vipyta.

R. Na nchi itageuka.

Tuombe: Mungu Baba yetu, Shush mapaj i ya Roho wako Mtakatifu dun iani kote. Ulimtuma Roho kwa Kanisa lako kuanzisha mafundisho ya habari njema: twaomba huyu Roho azidi kufanya kazi uiimwenguni kupitia nyoyo za wote wanaoamini. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

V. Wewe, Bwana wangu utafungua mdomo wangu.

R. Na ulimi wangu utakusifu.

V. Mungu kubuwa kunisaidia.

R. Unisaidie sasa hivi.

V. Atukuzwe Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu.

R. Kama mwanzo na sasa na siku zote na milele. Amina.

Halafu yanafuata makumi matano ya Rosari na Salamu Malkia.

Salamu Malkia Mama mwenye huruma; Salamu kwako twapata uzima, ndiwe mwenye kutuletea kitulizo. Ndiwe ambaye tunakutumainia sisi wana maskini wa Hawa. Twakungoja kwa kulia ni kulalamika chini hapa kwenye machozi. Haya basi, mwombezi wetu, utuelekezee macho yako kwa huruma. Tutakapotoka ugenini hapa, tufanyizie twende kumwangalia Yesu, mzao mbarikiwa wa tumbo lako. Ee Bikira Maria mwenye huruma, Ee Bikira mwema, Ee Bikira mpole.

V. Utuombee, Mzazi Mtakatifu wa Mungu.

R. Tujaliwe ahadi za Kristo.

Tuombe: Ee Mungu, ambae Mwanao wa pekee ametupatia Ukombozi milele kwa kuzaliwa, kufa na kufufuka kwake; twaomba utufanyizie sisi tuliofikiri juu ya matendo hayo ya Rosari Takatifu, tupate nguvu za kufuata mafundisho vote yaliyomo na kupewa maagano yake kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

V. Moyo Mtakatifu wa Yesu R. Utuhurumie.

V. Moyo wa Maria wenye usaf R. Utuombee.

V. Yosefu Mtakatifu R. Utuombee.

V. Yohani Mwinjili Mtakatifu R. Utuombee.

V. Ludoviko Mtakatifu wa Montfort R. Utuombee.

Kwjina la Baba.....

### KATENA YA LEJIO

Antiphonu. Nam huyu binti atokaye kama alfajiri, mzuri kama mwezi, ana nuru kama jua, anatisha kamajeshi lililo tayari kupigana?

+ Moyo wangu wamtukuza Bwana.

Na Roho yangu imeshangilia katika Mungu

Mkombozi wangu.

Kwa kuwa ameungangalia unyenyekevu wa mtumishi wake; toka sasa vizazi vyote watanisifu mwenye heri.

Kwani amenitenda makubwa aliye Mwenyezi, na jina lake takatifu.

Na huruma yake ipo toka kizazi hata kizazi kwa wale wenye kumcha.

Ameonyesha enzi kwa mkono wake.

amewatawanya wenyewe kiburi miyoni mwao.

Amewaondosha wenyewe enzi katika kiti, akawakuza wanyenyekevu.

Wenye raja amewashibisha mema,

matajiri akawarudisha mikono mitupu.

Amempokea Isreal mtumishi wake, akikumbuka huruma yake.

Kama aliyowaambia baba zetu;

Ibrahimu na wazao wake hata rnilele.

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Kama mwanzo na sasa na siku zote na milele.

Amina

Antiphonu. Nam huyu binti atokaye kama

alfajiri, mzuri kama mwezi, ana nuru kama jua, anatisha kamajeshi lililo tayari kupigana?

V. Ee Maria uliyembwa pasipo dhambi ya asili.

R. Utuombee sisi wenyewe kukimbilia kwako.

Tuombe: Ee Bwana Yesu Kristo, uliyempanishi wetu kwa Mungu Baba na uliyekubali kumteua Mama yako Bikira Maria kuwa Mama yetu, pia na Mpatisi wetu kwako, tunakuomba kila anayekuwa kuomba wema wako umjalie na afurahi kuupokea kwa kupitia kwake. Amina.

### SALA ZA MWISHO

Kwa jina la Baba .....

Tunakimbilia ulinzi wako Mzazi Mtakatifu wa Mungu, usitunyime tukiomba katika shida zetu, utuokoe siku zote tuingiyo hatarini, ewe Bikira mtukufu mwenye baraka. Amina.

V. Maria uliyekingiwa dhambi ya asili, mtoaji

wa neeroa zote

(au Jina la Praesidium) R. Utuombee

V. Mach Mtakatifu, na Gabriel Mtakatifu R. Utuombee

V. Enyi nguvu za mbinguni Malaika wa Jeshi

la Maria R. Utuombee.

V. Yohani Mbatizaji Mtakatifu R. Utuombee.

V. Petro na Paulo Watakatifu R. Utuombee.

Ee Mungu Mwenyezi utianUalie sisi tlolioingia katika Legio ya Maria, utujaze na moyo wa imani kwako na kumtunaini yeze ili tuweze kuishinda dunia. Tia ndani ya nyoyo zetu imani kuu pamoa na mapendo kusudi ya kufanya kazi zetu zote kwa ajili yako tu, na kumpenda jirani yetu kabisa na kumsaidia pia kwa ajili yako. Tunaomba imani ilio imara kama jabali isiyoweza kushindwa na matata ya dunia hii, au na mashaka mengine yote. Tunaomba imani kuu itakayotupa nguvu ya kumaliza mambo makubwa kwa ajili ya utukufu wako na kwa wokovu wa roho za wengino. Tunaomba imani yenye kutuongoza kwa umaja, tukiwasha kila mahali moto wa mapendo yako, kuwasaidia watu walio gizani na wakao ndani ya kivuli cha mauti, kuwapa nguvu wale wengine wanaotaka kulegea nao waliotenda dhambi kubwa kuwarudishia uzima. Tunaomba neema ya kutuongoza sisi wenye katika njia ya amani ili mwisho wa dunia, sisi sote tulio katika Lejio ya Maria tuingie usfalme wa Mungu wenyewe utukufu milele.

Amina

Roho za marehemu Walejio wetu, pamoa na roho za maoehernu wote, wapumzike kwa amani.

Arnina: Kwa jina la I3aba .....

(Kiswahili)

Cum Permissu Superiorum